

**ELIMU**
Waziri apongeza Equity Group Foundation kwa mpango wao wa Wings to Fly
UK 3



**AFYA**
Mpango wa kitaifa wa kudhibiti maambukizi ya Kansa kutatua changamoto ya gharama ya matibabu UK 4

**MAFUNZO**
Kaunti yazindua muundo wa mafunzo unaowapa wanafunzi mbinu za kuhakiki mada



UK 9


www.mygov.go.ke

JULAI 25, 2023

# MyGov.

TATHMINI YA WIKI

TOLEO No. 4/2023-2024


GARI MOSHI

# Ufanisi SGR ikisafirisha tani 26.3M za shehena miaka sita

Ripoti ya Utendaji ya SGR ya Usafirishaji kutoka kwa KR na Afristar inafichua rekodi ya kuvutia, inayoonyesha usafirishaji usio na visiki wa mbolea iliyoagizwa kwa ruzuku kwa wakulima kote nchini.



**NA MUTISHO MBITHI**
**(MYGOV)**

Shirika la Reli la Kenya (KRC) na Afristar, kampuni inayosimamia Reli ya Kisasa (SGR), zimepata ufanisi mkubwa kwa kusafirisha zaidi ya tani milioni 26.3 za mizigo kutoka nje kati ya Januari 2018 hadi Mei 2023.

Ufanisi huo, kulingana na taarifa kutoka kwa Shirika la Reli la Kenya na Afristar, inayosimamia SGR, linaonyesha jukumu muhimu lililofanywa na Reli ya Kisasa (SGR) katika kubadilisha usambazaji wa mizigo na kusaidia maendeleo ya kilimo nchini kote.

Ripoti ya Utendaji wa SGR ya Usafirishaji kutoka kwa KR na Afristar inafichua rekodi ya kuvutia, inayoonyesha usafirishaji usio na vizingiti wa mbolea iliyoagizwa kwa ruzuku kwa wakulima kote nchini.

Ripoti hiyo inasema kuwa katika kipindi cha miezi miwili pekee iliyopita, tani 34,400 za mbolea zilisafirishwa kutoka bandari ya Mombasa hadi kituo cha Athi River, na hivyo kuhakikisha inatolewa kwa wakati.

Ripoti hiyo inaongeza kusema kwamba kwa hisani ya utendakazi wa mtandao wa reli zinazounganishwa nayo, SGR iliwezesha usafirishaji wa mbolea kwa mabehewa ya reli ya zamani (MGR) katika kituo cha Mai Mahiu, na kuwezesha usambazaji wake katika maeneo ya watumiaji

ENDELEA UK 2

# KTDA yazindua SMS kwa wakulima kufuatilia malipo yao

**NA WANGARI MWANGI**
**(KNA)**

Zaidi ya wakulima 650,000 wa mashamba madogo wa chai walio chini ya Shirika la Maendeleo ya Chai Kenya (KTDA) sasa wataweza kufuatilia malipo yao ya majani chai baada ya shirika hilo kuzindua apu ya simu, Huduma ya Ujumbe Mfupi (SMS) na jukwaa la Data ya Huduma ya Ziada (USSD) ili kuboresha mawasiliano.

Kupitia majukwaa haya, wakulima wa chai pia wataweza kupokea taarifa za kila siku, wiki na mwezi kuhus uzani wa chai iliyovunwa inayopelekwa viwandani na pia kupata huduma za nyanjani.

Kulingana na Mkurugenzi Mkuu wa Huduma za Usimamizi wa KTDA Bw. Julius Onguso, kwa mara ya kwanza tangu serikali ilipoanzisha mpango wa mbolea ya ruzuku mwaka wa 2022, wakulima wa

ENDELEA UK 2

# Wakenya wang'aa katika Diamond League




Mtimuaji mbio kwa kasi zaidi Kenya na Afrika, Ferdinand Omanyala ashinda mbio za mita 100 nchini Monaco.



KULIA: Faith Kipyego avunja rekodi yake ya tatu ndani ya siku 50 katika Wanda Diamond League, Monaco.

**Takwimu za Wiki**

**40**
Nchi wanachama zinazoshiriki katika uchaguzi wa Katibu Mkuu wa International Maritime Organization

**360m**
Gharama ya maabara ya kisasa ambayo serikali ya Japan ikishirikiana na Mt. Kenya University imeanzisha.

**2050**
Mwaka ambapo inakadiriwa theluthi mbili ya watu duniani watakuwa wanaishi katika sehemu za miji

**50,000**
Idadi ya miti ya



maembe ambayo Kerio Valley Development Authority (KVDA) itasambaza katika eneo la Tot, wodi ya Endo.

**23,000**
Wahalifu wa makosa madogo ambao wameachiliwa na idara ya kurekebisha tabia kwa lengo la kupunguza msongamano wa wafungwa kwenye magereza

# Ufanisi SGR ikisafirisha tani 26.3m za shehena ndani ya miaka sita

ENDELEA KUTOKA UK 1



waliokusudiwa.

"Kwa kutumia mitandao yote miwili ya SGR na MGR, KRC imehakikisha kuwa inasambaza mizigo mbalimbali kwa wakati, ikiwa ni pamoja na bidhaa za kawaida kama vile ngano, klinka ya saruji, sukari, chai, mchele na lami na kiasi cha mizigo ya kawaida inayosafirishwa kimeshuhudia ukuaji mkubwa, na hivyo kusisitiza zaidi ufanisi wa SGR.

Utendakazi huu mzuri, ripoti inasema, ni matokeo ya ushirikiano wa karibu kati ya mashirika muhimu ya serikali, ikiwa ni pamoja na KRC, Mamlaka ya Bandari ya Kenya (KPA), Mamlaka ya Ushuru ya Kenya (KRA), na mashirika mengine yanayohusika na mizigo. Taarifa ya Afristar na KR inaongeza kuwa juhudi za pamoja za uuzaji, ndani na katika masoko ya usafirishaji, zimedumishwa kupitia ushirikiano wa mara kwa mara na washikadau muhimu. Hasa, ziara ya hivi majuzi ya maafisa kutoka Wizara ya Uchukuzi ya Uganda ilionyesha uunganishaji wa mizigo usio na vizingiti unaowezeshwa na mitandao ya reli ya SGR na MGR, na hivyo kuimarisha zaidi biashara ya kikanda. Ili kukabiliana na idadi inayoongezeka, ripoti hiyo inasema, KRC na Afristar zimeongeza matumizi ya mabehewa yote 1620 yaliyopo na kuhakikisha muda wa na uhusiano wakimkakati kati ya mtandao wa SGR na MGR umerahisisha uwasilishaji wa mizigo, haswa kuelekea Malaba-Kampala.

Hasa, taarifa inasema kuwa hatua hiyo muhimu iliafikiwa mnamo Julai 2021 wakati treni ndefu iliyojumuisha mabehewa 75 ilipozinduliwa, na kuongeza maradufu uwezo wa usafiri hadi tani 150.

# KTDA yazindua nambari ya SMS wakulima kufuatilia malipo yao

ENDELEA KUTOKA UK 1



**Wafanyakazi wachuma majani chai katika shambani eneo la Chinga, Othaya, kaunti ya Nyeri. KTDA imezindua apu na nambari ya SMS kuimarisha mawasiliano kati ya shirika hilo na wakulima wenye mashamba madogo. Picha: Wangari Mwangi/KNA**

chai sasa wataweza kuuliza kuhusu malipo ya mbolea.

Onguso alisema kuanzishwa kwa Apu ya wakulima ya KTDA, SMS na majukwaa ya USSD ni sehemu ya ajenda ya mageuzi ambayo yanalenga kutoa uwazi na uwajibikaji kwa kuwapa wakulima hali kamili ya hali ya akaunti zao.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa utoaji wa mbinu mbalimbali utawahakikishia wakulima uwezo wa kufikia hali ya akaunti zao kwenye simu zao za mkononi. "Hii inaashiria mabadiliko ya kidijitali ya utoaji wa huduma za KTDA kwa wakulima wake ambayo tunaamini yatasaidia sana kufikia ufanisi endelevu," alisema katika taarifa kwa vyombo vya habari. Apu hiyo ambayo ilijaribiwa katika viwanda vinane kabla ya kuanzishwa itatoa taarifa kuhusu huduma mbalimbali za KTDA kwa wakulima waliosajiliwa. Kwa upande mwingine, nambari ya usajili ya SMS 20213 itarahisisha mawasiliano ya moja kwa moja kati ya mkulima na kiwanda. Wakulima pia wameshauriwa kutumia *302# kuuliza kuhusu utoaji wa majani chai, hali ya malipo ya majani yanayowasilishwa na utoaji wa mbolea. "Kwa kukumbatia na kutumia teknolojia ili kuboresha mawasiliano na ushirikiano wetu na wakulima wetu, tunaamini kwamba hii itaongeza uwazi na uaminifu wa shughuli zetu zote kwa wakulima," alisema Onguso.

REPUBLIC OF KENYA

## HUDUMA YA KITAIFA KWA VIJANA

## TANGAZO LA ZABUNI

### USAMBAZAJI NA UWASILISHAJI WA MAFUTA NA VILAINISHAJI NA YA ZABUNI. NYS/PROC/31/2023-2025

**HUDUMA YA KITAIFA KWA VIJANA (NYS)** inakaribisha zabuni zilizofungwa kutoka kwa wazabuni wanaostahiki kwa usambazaji na uwasilishaji wa Mafuta na Vilainishaji -Zabuni ya kazi ya Mfumo (Zabuni Huria) kwa miaka 2.

Seti kamili ya hati za zabuni inaweza kupakuliwa kutoka kwa tovuti za Huduma: **www.nys.go.ke** au kutoka Tovuti ya Wizara ya Fedha: **http//supplier.treasury.go.ke** ***bila malipo*** au Ksh.1,000 zitatozwa kwa kupata hati ya zabuni kutoka makao makuu ya NYS inayolipwa kwa pesa taslimu ya NYS au hundi ya benki.

Bei zilizonukuliwa zinapaswa kujumlisha ushuru wote, lazima ziwe katika Shilingi za Kenya na zitaendelea kuwa halali kwa siku (120) kuanzia tarehe ya kufungwa ya zabuni. Wazabuni watatoa dhamana ya Zabuni ya Kshs. 1,000,000 halali kwa siku 120 kuanzia tarehe ya ufunguzi wa Zabuni.

Hati zilizokamilishwa za zabuni zinapaswa kuambatanishwa katika bahasha iliyofungwa iliyo na nambari ya zabuni na kuwekwa kwenye Sanduku la Zabuni katika Makao Makuu ya NYS, Ruaraka, orofa ya 1 ili kupokelewa mnamo au kabla ya tarehe **8 Agosti 2023 saa 10.00 asubuhi** na kutumwa kwa:

**KAIMU MKURUGENZI MKUU/CEO**
**MAKAO MAKUU YA HUDUMA YA VIJANA KWA TAIFA**
**P. O. Box 30397-00100**
**NAIROBI.**

Zabuni zitafunguliwa mara moja baada ya hapo saa 10.00 asubuhi mbele ya Wazabuni au wawakilishi wao watakaoamua kuhudhuria katika Makao Makuu ya NYS, Ruaraka.

**MKUU, USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MFUMO WA USAMBAZAJI**
**KWA: KAIMU MKURUGENZI MKUU**

KENYA VISION 2030

*In Search of Better Health*

## KENYA MEDICAL RESEARCH INSTITUTE

### INVITATION TO TENDER

The Kenya Medical Research Institute (KEMRI) is a state corporation, established through the Science and Technology (Amendment) Act of 1979. Its mandate is to conduct research in human health. KEMRI wishes to procure the following.

| TENDER NUMBER | TENDER DESCRIPTION | BID BOND AMOUNT | OTHER DETAILS |
|---|---|---|---|
| KEMRI/RFP/001/2023-2024 | Request for Proposal for provision of recruitment consultancy services for position of;<br>• Director General /CEO<br>• Director Corporate Services KMR 2 and Deputy Director Human Resource Management KMR 3 | N/A | Open |

Interested eligible and qualified tenderers with relevant experience in similar undertakings are invited to submit their bids. The tender documents may be obtained from the procurement department, KEMRI, headquarters off, Mbagathi way, P. O. Box 54840 - 00200 Nairobi during normal working hours upon payment of a non-refundable fee of Ksh.1,000.00 per set of documents to be deposited in:

**Bank:** **Kenya Commercial Bank,**
**Branch:** **Kipande House,**
**Name:** **Kenya Medical Research Institute, Main Account**
**Account Number:** **1104161362**

Alternatively, Tender documents can be downloaded free of charge from our website ***www.kemri.go.ke***

However, candidates who choose to download the documents must notify the procurement office immediately for record purposes by email: ***procurement@kemri.go.ke***

The bid shall be a single package consisting of two separate envelopes, containing the financial and the technical proposals: as per tender. The envelopes shall be marked as **"FINANCIAL PROPOSAL" AND "TECHNICAL PROPOSAL"**, separately, as per tender. In the first instance, the "Technical Proposal "shall be opened and the envelope marked as "Financial Proposal" shall be retained unopened in the custody of the procuring agency: The procuring agency shall evaluate the technical; proposal in the manner prescribed in advance, without reference to the price and shall reject any proposal which does not conform to the specified requirements;

The envelope containing the tender document, bearing no indication of the bidder and clearly marked as indicated in the table above, should be deposited in the tender box at the Reception Area, Ground Floor, KEMRI Headquarters or sent by post to:-

The Director/CEO
Kenya Medical Research Institute
P. O. Box 54840- 00200
Nairobi

So as to reach not later than Tuesday, 8th AUGUST 2023 at 10.00am local time. Interested bidders or their representatives are invited to witness the opening of the bids, to be held at the, Conference Hall, at KEMRI Headquarters on the same day.

KEMRI may terminate the procurement proceedings prior to entering into a contract and reserves the right to accept or reject any or all tenders, without being bound to give reasons for its decision or incurring any liability. The Institute is also not obligated to award to the firm that offers the lowest price.

**DIRECTOR GENERAL/CEO,**

**KENYA MEDICAL RESEARCH INSTITUTE**

# Waziri asifu mpango wa Wings to Fly wa Equity Group

**NA HAMDI MOHAMUD (KNA)**

Waziri wa Elimu Ezekiel Machogu amepongeza Wakfu wa Equity Group (EGF) kwa kuwezesha mamia ya wanafunzi kutoka familia maskini kupata elimu ya sekondari na ya juu.

Bw Machogu alisema Mpango wa masomo wa shirika hilo wa Wings to Fly, umewezesha wanafunzi wengi kutoa michango muhimu ndani na nje ya nchi kama wataalamu katika nyanja tofauti.

Waziri alisema hayo wakati Afisa Mkuu Mtendaji wa EGF, Dkt James Mwangi alipomtembelea ofisini kwake.

Waliohudhuria hafla hiyo ni Katibu wa Idara ya Serikali ya Elimu ya Msingi, Dkt Belio Kipsang na Katibu wa Idara ya Elimu ya Juu na Utafiti Dkt Beatrice Muganda Inyangala.

Dkt Mwangi aliishukuru serikali kwa usaidizi inayopatia EGF, akisema



Waziri wa Elimu, Ezekiel Machogu

msaada huo umeiwezesha kutoa ufadhili wa masomo kwa mamia ya watoto

> Mpango huo umesaidia wanafunzi kutoa mchango mkubwa nchini na hata kimataifa-Waziri

kwa miaka mingi tangu ulipoanzishwa.

Alisema baadhi ya wanafunzi 17,000 wamepata elimu ya chuo kikuu na kati yao 3,400 tayari wamemaliza elimu ya chuo kikuu.

Mwangi alisema wanafunzi 871 wamepata ufadhili wa masomo katika vyuo vikuu nchini Amerika, huku 218 kati yao wakiwa katika vyuo vikuu vya Ivy nchini Amerika.

Dk Mwangi alisema wakfu huo umeunda mpango wa kusaidia wanafunzi ambao hawajafikisha alama za kujiunga na chuo kikuu kupata ufadhili wa kusomea kozi katika vyuo vya Ufundi.

Dkt Kipsang alisema mpango huo, ambao sasa umetimiza mwaka wake wa kumi na tano, umebadilisha maisha ya mamia ya watoto na akaishukuru EGF kwa ufadhili huo.

Dkt Inyangala aliomba EGF kushirikiana na serikali kutoa mafunzo kwa wakufunzi akisema mafunzo hayo yataimarisha uwezo wao wa kutoa uzoefu wa mafunzo ya kiwango cha juu kwa wanafunzi wanaofanya kozi katika TVET.

Mpango wa ufadhili wa Wings to Fly, ambao ni mpango wa Equity Group na Mastercard Foundation (MCF), unasaidia watoto kutoka familia za mapato ya chini wanaofanya vyema katika mitihani kujiunga na elimu ya sekondari.

# Kitengo cha Utekelezaji wa Huduma Serikalini chaimarishwa

**NA GEORGE KAIGA (KNA)**

Serikali ya Kitaifa imeimarisha kitengo cha Utekelezaji wa Huduma Serikali (GDS) ili kuharakisha ukamilishaji wa Miradi ya Serikali ya Kitaifa, mipango na sera zenye manufaa makubwa kwa wananchi.

Akiongoza kikao cha kwanza cha Kamati ya Kitaifa ya Uratibu na Usimamizi wa Utekelezaji wa Maendeleo ya Serikali cha kanda (NGD-RICMC) mjini Kakamega, Mkuu wa eneo la Magharibi Bw Samson Macharia alisema kamati hiyo inawaleta pamoja wakuu wote wa eneo wa wizara, idara na mashirika (MDAs).

Kamishna wa eneo alisema mikutano kadhaa ya Maendeleo na Kuthibitisha Miradi itafuata kwa wakati ufaao katika eneo lote la Magharibi, akiongeza kuwa Kamati za Uratibu na Usimamizi za Kaunti pia zitazinduliwa.

"Wakuu wote wa Wizara na Idara za Serikali lazima waandae ripoti za miradi, mipango na sera wanazozitekeleza kwa kuwa kamati itakuwa ikitembelea mara kwa mara miradi kadhaa ili kutathmini maendeleo," aliagiza.

"Tutaamua ni miradi gani ya kutembelea, kufuatilia na kutathmini na kutatua baadhi ya changamoto zinazoikabili na kuzipeleka kwenye kamati ya Makatibu(PSs) ili kuharakisha kukamilika kwake," aliongeza. "Kamati inaongozwa na Mkuu wa eneo na wajumbe wanajumuisha Wizara, Idara na mashirika yote (MDAs), Mashirika ya wa Serikali yanayojimamia (SAGAs) huku Mkurugenzi wa eneo (GDS) akiongoza Sekretariati," alisema.

Katika kikao hicho, wajumbe walielezwa vyombo mbalimbali vya kisheria vikiwemo miongozo ya Uratibu wa Sera, Mipango na Miradi ya Serikali ya Kitaifa miongoni mwa vingine.

REPUBLIC OF KENYA

## PUBLIC SERVICE COMMISSION

**Our Vision**
*"A citizen-centric public service"*

**Our Mission**
*"To reform and transform the public service for efficient and effective service delivery"*

### RECRUITMENT OF INTERNS FOR GOVERNMENT MINISTRIES, DEPARTMENTS AND AGENCIES

The Public Service Internship Programme (PSIP) is a Government youth empowerment programme whose main objective is to offer college graduates the opportunity to gain hands-on experience and build skills in order to enhance their chances for employment, networking and entrepreneurship.

The Public Service Commission (PSC) is pleased to announce the recruitment of **8,000** interns (Cohort 6) under PSIP for the Financial Year 2023/2024.

**Requirements for Appointment**

For appointment to an internship position, a candidate must:

- Have a **Bachelor's degree** in any discipline from a recognized university;
- Have graduated not earlier than the year **2017**; and
- Be proficient in computer skills.

**Internship Duties and Responsibilities**

Duties include, but not limited to;

i. Completing duties mutually agreed upon and assigned by the supervisors;
ii. Documenting relevant skills acquired in their areas of deployment; and
iii. Actively participating in any relevant mentorship activities and additional responsibilities designed for the programme.

**Duration Of internship**

Twelve (12) months- Non renewable

**Stipend**

The interns will be paid a stipend at a rate as determined by the Government.

**Certificate**

On successful completion of the Internship Programme, the interns will be awarded a certificate.

Interested and qualified graduates are requested to make their applications through the Commission's job portal accessible through **www.publicservice.go.ke** or **www.psckjobs.go.ke** by **14th August, 2023.**

***The Public Service Commission is an Equal Opportunity Employer***

**SECRETARY/CEO**
**PUBLIC SERVICE COMMISSION**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

## MINISTRY OF INVESTMENTS, TRADE AND INDUSTRY

***State Department for Industry***

### ADVERTISEMENT FOR VACANT POSITIONS

The State Department for Industry wishes to recruit qualified candidates to fill the following vacant positions:

| S/No. | Post | Grade | Terms of Service | Number of Vacancies |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Senior Industrial Development Officer | CSG 9 | Permanent and Pensionable | 40 |
| 2. | Principal Instructor | CSG 8 | Permanent and Pensionable | 8 |
| 3. | Senior Instructor | CSG 9 | Permanent and Pensionable | 8 |
| 4. | Instructor I | CSG 10 | Permanent and Pensionable | 8 |

Requirements and other detailed information for the above posts is available on the State Department's website **www.industrialization.go.ke**

Interested and qualified candidates are requested to make their applications by completing **ONE** application form **(PSC 2 form Revised 2016)**, CV, copies of academic and professional certificates and submit the same to the address below by post or hand delivery to **NSSF Building, Block B, 11th floor Room 1121** on or before **22nd August, 2023.**

The application form can be downloaded from the Public Service Commission website **www.publicservice.go.ke** or the State Department for Industry website **www.industrialization.go.ke**

**The Principal Secretary**
**State Department for Industry**
**P.O Box 30547-00100**
**NAIROBI**

KENYA VISION 2030

# Mpango wa kitaifa wa kudhibiti kansa kutatua gharama ya juu ya matibabu

NA PEACE MUTHOKA NA LUCY GATEI (KNA)




**Dkt Iheoma Onuekwusi, Mkuu wa Kitengo cha Magonjwa yanayoambukizwa na yasiyoambukizwa katika WHO-Kenya wakati wa uzinduzi wa mpango wa kitaifa wa kudhibiti kansa (NCCP) 2023-2027.**

Wizara ya Afya (MoH) imezindua Mpango wa Kitaifa wa Kudhibiti Saratani (NCCP) 2023–2027 ambao utaiongoza nchi kupatia kipaumbele hatua za kuzuia na kudhibiti saratani kwa kuzingatia mzigo uliopo wa ugonjwa huo na hatari zake zinazohusiana na mazingira na rasilimali zilizopo.

Waziri wa Afya Dkt Susan Nakhumicha alisema mpango wa utafiti wa uthibiti ni muhimu sana kwani ni Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Saratani nchini.

"NCCP inadhihirisha kuwa Serikali imejitolea kudhibiti na kuzuia saratani. Katiba ya Kenya na ajenda ya kuanzia mashinani inalenga kutoa Huduma ya Afya kwa Wote kwa Wakenya wote," alisema Nakhumicha.

Katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Katibuwa Idara ya Kitaifa ya Huduma za Matibabu Bw. Harry Kimtai, Dkt Nakhumicha alisema mpango uliozinduliwa unaoana vyema na Ruwaza ya 2030 ya Kenya.

"Kuna gharama kubwa ya matibabu ya saratani na viwango vya chini vya maisha nchini. NCCP itaimarisha sekta ya afya na kujenga ufahamu wa umma kuhusu saratani," alibainisha.

Kulingana na Waziri, Wizara imefurahishwa na hatua kubwa iliyofikia kuelekea saratani na hadithi nyingi za mafanikio kuhusu ushirikiano.

Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) nchini Abdourahmanne Diallo alisema kuwa WHO inaendelea kuunga mkono nchi wanachama ili kukuza sera, mipango ya kitaifa ya kudhibiti saratani ambayo inawiana na mikakati ya Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza na masuala mengine ya kiafya yanayohusiana nayo.

Kama shirika la kiufundi, Diallo alitangaza kwamba WHO iliweka kanuni na viwango vya udhibiti wa saratani ikiwa ni pamoja na ukuzaji wa kinga kulingana kwa kugunduliwa mapema, uchunguzi, matibabu, na mpango wa utunzaji wa wagonjwa na walioponа, na pia kukuza ufuatiliaji na tathmini kupitia sajili za saratani na utafiti ambao unalingana na mzigo wa ugonjwa wa eneo na rasilimali zinazopatikana.

"Kati ya asilimia 30 hadi 50 ya visa vyote vya saratani vinaweza kuzuilika na sote tunajua kuwa kinga hutoa mkakati wa muda mrefu wa kudhibiti saratani. WHO inatoa msaada kwa nchi wanachama katika kuimarisha sera na mipango ya kitaifa ya kuongeza ufahamu na, kupunguza uwezekano wa hatari za saratani kwa kufuata mitindo mizuri ya maisha, "aliongeza.Diallo, katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Mkuu wa kitengo cha magonjwa ya Kuambukiza na Yasiyo ya Kuambukiza katika WHO Kenya, Dkt Iheoma Onuekwusi, alisema kuwa WHO inafanya kazi na serikali kuhakikisha matibabu bora ya saratani yanapatikana na kuhimiza upatikanaji na bei nafuu za dawa salama na bora, chanjo, na uchunguzi wa saratani ambao ni muhimu kwa magonjwa yanayoweza kuepukika na magonjwa mengine yasiyoweza kuepukika. "Kwa pamoja tunaweza kukuza maisha yenye afya, kuzuia saratani, kuweka hatua za kutambua mapema, kutibu ipasavyo na kuponya saratani, na kutoa maisha bora kupitia utunzaji wa matibabu," Diallo alisisitiza.

# Serikali yazindua mpango wa miaka mitano wa mlo shuleni eneo la North Rift

NA CAROLYNE CHERONO (KNA)



**Waziri wa Ulinzi, Adan Duale akiandamana na Gavana Benjamin Cheboi, Kamishna wa Kaunti Stephen Kutwa na Mbunge wa eneo hilo William Kamket wakati wa ukaguzi wa miradi ya ujenzi wa shule kaunti ndogo ya Tiaty West.**

Serikali ya Kitaifa itaendesha mpango wa miaka mitano wa lishe shuleni ili kusaidia shule za msingi na upili katika maeneo yenye ukosefu wa usalama eneo la Kaskazini mwa Bonde la Ufa.

Waziri wa Ulinzi Adan Duale alisema wizara yake itatoa chakula kila mwaka kupitia kambi za Jeshi la Ulinzi la Kenya (KDF) kwa shule zote zilizoathirika, kukarabati madarasa pamoja na ujenzi wa bweni katika shule ya msingi ya Chesitet, shule ya msingi ya Kositei na Shule ya Upili ya Kapedo katika kaunti ndogo ya Tiaty Magharibi, Kaunti ya Baringo ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanabaki shuleni.

Duale ambaye aliandamana na Gavana Benjamin Cheboi, Kamishna wa Kaunti Stephen Kutwa na Mbunge wa eneo hilo William Kamket alikuwa akizungumza wakati wa ukaguzi wa miradi ya ujenzi katika shule hizo tatu ambapo ukarabati unatazamiwa kukamilika mwishoni mwa Agosti mwaka huu. Alibainisha kwa wasiwasi kwamba kiwango cha wanafunzi kilikuwa cha chini kabisa kutokana na ukosefu wa usalama kama Shule ya Msingi ya Chesitet ambayo wanafunzi ni 87 pekee.

"Tunataka watoto katika Shule ya Msingi ya Chesitet waongezeke hadi zaidi ya 300 na kupitia KDF tutajenga madarasa zaidi na kudumisha mpango wa kuwalisha shuleni ili watoto wengi wabaki shuleni," Duale alisema.

Waziri huyo pia aliwataka wazazi kuhakikisha watoto wengi zaidi wanapelekwa shuleni kwani ni haki yao na serikali imejitolea kuhakikisha kuwa maeneo yenye ujangili katika kaunti ndogo za Baringo Kaskazini, Baringo Kusini na Tiaty Mashariki na Magharibi yatanufaika na mpango wa mlo shuleni ili kuhakikisha wanapata elimu.

Kuhusu afya, Waziri alisema akina mama na watoto wanastahili kupokea huduma za afya katika kambi za KDF za Chesitet ili kuepuka kupoteza maisha.

"Wahalifu hawatapewa matibabu katika kambi za KDF na ninataka kuhimiza kila mkazi kusalimisha bunduki zote haramu tunapopanga kupeleka Polisi wa Akiba kusaidia katika kudumisha usalama," Duale alisema.

Gavana Cheboi alisema serikali ya kaunti itaajiri walimu zaidi wa Elimu ya Chekechea (ECDE) na kutumwa katika shule hizo kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata elimu bora kama wa kaunti nyingine ndogo.

REPUBLIC OF KENYA

## WIZARA YA KILIMO NA USTAWISHAJI WA MIFUGO

### MWALIKO WA MAONI NA MAWASILISHO KUHUSU RASIMU YA MSWADA WA PARETO (MAGEUZI), 2023

Sheria ya pareto, 2013 ilitungwa pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Kilimo na Chakula (Na. 13 ya 2013) na Sheria ya Mazao (na. 16 ya 2013). Miswada yote mitatu iliidhinishwa na Rais tarehe 14 Januari, 2014.

Sheria ya Mamlaka ya Kilimo na Chakula, 2013 na Sheria ya Mazao, 2013 zilikusudiwa kudhibiti mazao yote yaliyopangwa wakati Sheria ya Pareto, 2013 ilitungwa kudhibiti Pareto, na hivyo kuleta mgongano. Kifungu cha 3 cha Sheria ya Pareto, 2013, kinaanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Pareto huku Kifungu cha 4 kinaeleza majukumu yake. Majukumu ya Mamlaka ya Kilimo na Chakula yanafanana na yale ya Mamlaka ya Kilimo na Chakula iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 3 cha Sheria ya Mamlaka ya Kilimo na Chakula, 2013.

Ili kukabiliana na mgongano kati ya masharti ya Sheria ya Pareto, 2013 na Sheria ya Mamlaka ya Kilimo na Chakula ya mwaka 2013, jedwali la kwanza la Sheria ya Mamlaka ya Kilimo na Chakula ya mwaka 2013 lilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Miscellaneous Amendments) (Na 7 ya mwaka 2016) kwa kuingiza Taasisi ya Mamlaka ya Kilimo na Mafanikio ya Pareto. Ingawa marekebisho yalihusu kubatilishwa kwa Sheria ya Pareto, 2013, Sheria hiyo haijabatilishwa kabisa, ambayo rasimu ya Mswada wa Pareto (Mageuzi) wa 2023 itafanya kazi.

Mswada huo utabatilisha Sheria ya Pareto, 2013 ili kuondoa mgongano wa kimaslahi uliopo katika sekta ndogo ya pareto na kushughulikia urudufu wa sheria, miongoni mwa maeneo mengine muhimu ya mada.

Wadau wa sekta na wananchi wanaalikwa kuikosoa/kupitia rasimu ya Mswada huo ili kuhakikisha kuwa ni rahisi na masuala yao yote yanashughulikiwa. Tafadhali pata rasimu kutoka kwa viungo vifuatavyo;

- **https://www.agricultureauthority.go.ke/index.php/en/**
- **https://kilimo.go.ke/**

Maoni yaliyoandikwa yanakaribishwa na yanaweza kuwasilishwa kupitia anwani zifuatazo:

**Katibu**
**Idara ya Ustawishaji wa Mazao**
**Wizara ya Kilimo na Ustawishaji wa Mifugo**
**Kilimo House, Cathedral Road**
**S.L.P 30028**
**Nairobi.**
Au kwa Barua Pepe: **psagriculture@kilimo.go.ke**

**Mkurugenzi Mkuu**
**Mamlaka ya Kilimo na Chakula**
**Tea House, Barabara ya Naivasha, kando na Barabara ya Ngong**
**S.L.P 37962-00100**
**Nairobi.**
Au kwa Barua Pepe: **info@afa.go.ke**

Ufafanuzi kuhusu Mswada huo unaweza kuombwa kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Kilimo na Chakula (AFA) **+254-722200556/734600944**

Maoni yako yatasaidia sana katika kuhakikisha kuwa mfumo wa kisheria wezeshi unaanzishwa kwa ajili ya sekta ya Pareto.

**MITHIKA LINTURI,**
**WAZIRI**
**WIZARA YA KILIMO NA USTAWISHAJI WA MIFUGO**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

KIPI
Kenya Industrial Property Institute

**VISION**
**A world class institution in administration of industrial property rights**

**MISSION**
**To protect and promote industrial property rights and foster innovation for sustainable development in Kenya**

# RECRUITMENT OF MANAGING DIRECTOR

Kenya Industrial Property Institute (KIPI) is a State Corporation under the Ministry of Investments, Trade and Industry. The Institute's mandate as provided for under the Industrial Property Act, No. 3 of 2001 and the Trade Marks Act, Cap 506 is to promote inventive and innovative activities, facilitate the acquisition of technology through registration and regulation of patents, utility models, technovations, industrial designs and trade marks.

In implementing the Government Bottom-Up Economic Transformational Agenda (BETA), KIPI wishes to recruit dynamic, result-oriented and self-driven person to fill the vacant position below: -

| MANAGING DIRECTOR | GRADE KP '1' (REF. NO. KIPI/ADM/HR/2023/1) | ONE (1) POSITION |
|---|---|---|

| | |
|---|---|
| **Terms of service** | **: Contract** |
| **Basic Salary** | **: Ksh. 260,000/= - Ksh. 460,000/= p.m** |
| **House Allowance** | **: Ksh. 80,000/= p.m** |
| **Entertainment Allowance** | **: Ksh. 65,000/= p.m** |
| **Medical Cover** | **: As per KIPI's medical policy** |
| **Leave Allowance** | **: As per KIPI Human Resource Manual** |
| **Annual Leave** | **: 30 working days per financial year** |

### (a) Duties and Responsibilities

Reporting to the Board, the Managing Director will be responsible for:

i. Providing strategic leadership and ensuring proper day to day management of the Institute;
ii. Ensuring implementation of Institute's programmes, project and activities;
iii. Implementing Board policies and decisions;
iv. Ensuring registration of patents, industrial designs, utility models, trade and service marks are done effectively and efficiently;
v. Implementing the Performance Contract signed between the Board and the Government;
vi. Implementing the provisions of the Industrial Property Act, 2001 and the Trade Marks Act, Cap 506;
vii. Preparing and coordinating business related proposals, reports and other submissions for consideration by the Board;
viii. Implementing the relevant local, regional and international agreements to which Kenya is a Party;
ix. Ensuring proper management and control of the Institute's financial and non- financial resources in an efficient and cost-effective manner in consultation with the Board, parent Ministry and all the relevant Government agencies and stakeholders;
x. Serving as Secretary to the Board;
xi. Carrying out other responsibilities necessary for the achievement of the Institute's objectives;
xii. Advising the Board on matters related to the implementation of the business of the Institute; and
xiii. Carrying out any other function directed by the Board from time to time.

### (b) Requirements for Appointment

i. A Master's Degree in Intellectual Property, Law, Science, Information Technology or Business Administration from a recognised university;
ii. A Bachelor's Degree in Law, Science, Information Technology or Business Administration from a recognised university;
iii. At least Seven (7) years working experience in matters relating to industrial property;
iv. Served at top management position for a minimum period of five (5) years;
v. Undergone senior management training for a minimum period of four (4) weeks from a recognised institution;
vi. Clear understanding of the role of industrial property rights in Kenya's socio- economic development;
vii. Must possess strong interpersonal skills;
viii. Must demonstrate good knowledge of public finance management and public procurement and asset disposal;
ix. Must have high degree of integrity and responsibility;
x. Membership to relevant professional body;
xi. Computer competence; and
xii. Must meet the requirements of Chapter 6 of the Constitution of Kenya, 2010.

The details of the position can be accessed on the Organization's website: **www.kipi.go.ke**

Interested and qualified persons are invited to make their applications by completing ONE Kenya Industrial Property Institute Application for Employment Form. The form may be downloaded from the Kenya Industrial Property Institute Website **www.kipi.go.ke**

The candidates should attach **COPIES** of the following documents to their application form:

- National Identity Card;
- Academic and Professional Certificates and Transcripts;
- Any supporting documents and testimonials;
- Letter of appointment to their current substantive post (where applicable);
- Letter of appointment to their previous post (where applicable);
- Equating degree certificates acquired from outside the country from the Commission for University Education; and
- Detailed Curriculum Vitae.

**Please Note:**

(i) KIPI is an equal opportunity employer and therefore, persons with disabilities (PwDs), the marginalized and the minorities are encouraged to apply.
(ii) Canvassing in any form will lead to automatic disqualification.
(iii) Successful applicants shall be required to submit clearance certificates from the following bodies at appointment level: -
  i. Higher Education Loans Board;
  ii. Kenya Revenue Authority;
  iii. Criminal Investigation Department; and
  iv. Ethics and Anti-Corruption Commission
(iv) Only shortlisted candidates will be contacted.

Completed application forms should be delivered to:

**The Chairman, Board of Directors**
**Kenya Industrial Property Institute**
**17 Kabarsiran Avenue, Lavington, Off Waiyaki Way**
**P.O. Box 51648-00200,**
**NAIROBI.**

So as to reach the Office of the **Chairman, KIPI Board of Directors** on or before **Monday, 14th August 2023 latest 5:00 P.M. (East African Time).**

**CHAIRMAN**
**BOARD OF DIRECTORS**
**KENYA INDUSTRIAL PROPERTY INSTITUTE**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

KIPI
Kenya Industrial Property Institute

# VACANCIES ANNOUNCEMENT

Kenya Industrial Property Institute (KIPI) is a State Corporation under the Ministry of Investments, Trade and Industry. The Institute's mandate as provided for under the Industrial Property Act, No. 3 of 2001 and the Trade Marks Act, Cap 506 is to promote inventive and innovative activities, facilitate the acquisition of technology through registration and regulation of patents, utility models, technovations, industrial designs and trade marks.

The functions of the Institute are to:

(a) Consider applications for, grant and registration of industrial property rights;
(b) Screen technology transfer agreements and licences;
(c) Provide to the public, industrial property information for technological and economic development;
(d) Promote inventiveness and innovativeness in Kenya; and
(e) Organize and conduct training, competitions and awards relating to industrial property matters.

In implementing the Government Bottom-Up Economic Transformational Agenda (BETA), KIPI wishes to recruit dynamic, result-oriented and self-driven persons to fill the vacant positions below: -

| S/ NO | POSITION | JOB VACANCY NO. | GRADE | NUMBER OF POSITIONS |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Deputy Managing Director, Technical Services | KIPI/ADM/HR/2023/2 | KP '2' | 1 |
| 2. | Manager, Research, Innovation and IP Information | KIPI/ADM/HR/RI/2023/3 | KP '3' | 1 |
| 3. | Manager, Finance and Accounts | KIPI/ADM/HR/FA/2023/4 | KP '3' | 1 |
| 4. | Human Resource Manager | KIPI/ADM/HR/2023/5 | KP '3' | 1 |
| 5. | Assistant Manager, Legal Services | KIPI/ADM/HR/LS/2023/6 | KP '4' | 2 |
| 6. | Assistant Manager, Finance and Accounts | KIPI/ADM/HR/FA/2023/7 | KP '4' | 1 |
| 7. | Assistant Manager, Supply Chain Management | KIPI/ADM/HR/SCM/2023/8 | KP '4' | 1 |
| 8. | Assistant Manager, Internal Audit | KIPI/ADM/HR/IA/2023/9 | KP '4' | 1 |
| 9. | Senior Patent Examiner | KIPI/ADM/HR/PA/2023/10 | KP '5' | 2 |
| 10. | Senior Accountant | KIPI/ADM/HR/FA/2023/11 | KP '5' | 1 |
| 11. | Senior Human Resource Officer | KIPI/ADM/HR/2023/12 | KP '5' | 1 |
| 12. | Senior Supply Chain Management Officer | KIPI/ADM/HR/SCM/2023/13 | KP '5' | 1 |
| 13. | Senior ICT Officer | KIPI/ADM/HR/ICT/2023/14 | KP '5' | 1 |
| 14. | Senior Strategy and Planning Officer | KIPI/ADM/HR/SP/2023/15 | KP '5' | 1 |
| 15. | Legal Officer | KIPI/ADM/HR/LS/2023/16 | KP '5' | 1 |
| 16. | Patent Examiner | KIPI/ADM/HR/PA/2023/17 | KP '6' | 2 |
| 17. | Trade Mark Examiner | KIPI/ADM/HR/TM/2023/18 | KP '6' | 2 |
| 18. | Accountant | KIPI/ADM/HR/FA/2023/19 | KP '6' | 2 |
| 19. | ICT Officer | KIPI/ADM/HR/ICT/2023/20 | KP '6' | 2 |
| 20. | Administration Officer | KIPI/ADM/HR/2023/21 | KP '6' | 1 |
| 21. | Principal Assistant Office Administrator | KIPI/ADM/HR/2023/22 | KP '6' | 2 |
| 22. | Librarian | KIPI/ADM/HR/RI/2023/23 | KP '7' | 1 |
| 23. | Accounts Assistant | KIPI/ADM/HR/FA/2023/24 | KP '7' | 1 |
| 24. | Senior Assistant Human Resource Officer | KIPI/ADM/HR/2023/25 | KP '7' | 1 |
| 25. | Senior Assistant Supply Chain Management Officer | KIPI/ADM/HR/SCM/2023/26 | KP '7' | 1 |
| 26. | Senior Assistant Office Administrator | KIPI/ADM/HR/2023/27 | KP '7' | 2 |
| 27. | Patent Assistant I | KIPI/ADM/HR/PA/2023/28 | KP '8' | 2 |
| 28. | Trade Mark Assistant I | KIPI/ADM/HR/TM/2023/29 | KP '8' | 1 |
| 29. | Assistant Office Administrator I | KIPI/ADM/HR/2023/30 | KP '8' | 1 |
| 30. | Senior Clerical Officer | KIPI/ADM/HR/2023/31 | KP '8' | 1 |
| 31. | Executive Driver | KIPI/ADM/HR/2023/32 | KP '8' | 1 |
| 32. | Trade Mark Assistant II | KIPI/ADM/HR/TM/2023/33 | KP '9' | 1 |
| 33. | Senior Driver | KIPI/ADM/HR/2023/34 | KP '9' | 2 |
| 34. | Senior Receptionist | KIPI/ADM/HR/2023/35 | KP '9' | 1 |
| 35. | Driver | KIPI/ADM/HR/2023/36 | KP '10' | 2 |
| | | **Total** | | **46** |

The details of the positions can be accessed on the Organization's website: **www.kipi.go.ke**
Interested and qualified persons are invited to make their applications by completing **ONE** Kenya Industrial Property Institute Application for Employment Form. The form may be downloaded from the Kenya Industrial Property Institute Website **www.kipi.go.ke**

The candidates should attach **COPIES** of the following documents to their application form:

- National Identity Card;
- Academic and Professional Certificates and Transcripts;
- Any supporting documents and testimonials;
- Letter of appointment to their current substantive post (where applicable);
- Letter of appointment to their previous post (where applicable);
- Equating degree certificates acquired from outside the country from the Commission for University Education; and
- Detailed Curriculum Vitae.

**Please Note:**

(i) KIPI is an equal opportunity employer and therefore, persons with disabilities (PwDs), the marginalized and the minorities are encouraged to apply.
(ii) Canvassing in any form will lead to automatic disqualification.
(iii) Successful applicants shall be required to submit clearance certificates from the following bodies at appointment level: -
  a. Higher Education Loans Board;
  b. Kenya Revenue Authority;
  c. Criminal Investigation Department; and
  d. Ethics and Anti-Corruption Commission
(iv) Only shortlisted candidates will be contacted.

Completed application forms should be **delivered** to:

**The Managing Director**
**Kenya Industrial Property Institute**
**17 Kabarsiran Avenue, Lavington, Off Waiyaki Way**
**P.O. Box 51648-00200, NAIROBI.**

So as to reach the Office of the Managing Director on or before **Monday, 14th August 2023 latest 5:00 P.M. (East African Time).**

**MANAGING DIRECTOR**
**KENYA INDUSTRIAL PROPERTY INSTITUTE**

KENYA VISION 2030

# World Vision and West Pokot County collaborate to protect children rights

BY RICHARD MUHAMBE AND MAURICE OSORE (KNA)

West Pokot County has trained Children Protection Volunteers (CPVS) in a bid to protect children against any forms of violation.

This initiative has been taken due to the large number of children's rights violations that occur especially in remote areas within the county where locals are either unwilling to report or are less informed about children's rights.

The Department of Children's Services in collaboration with World Vision Kenya took the initiative to train and empower CPVs from every ward with a huge percentage being drawn from Kasei and Sigor Wards.

"We have trained 33 Children Protection Volunteers (CPVs) who are from all the 20 wards in West Pokot County and a good number from Karsei and Sigor on how to solve or channel child abuse cases," stated West Pokot Children's Officer Mr. Fredrick Nyatige.

Nyatige outlined that early marriages, Female Genital Mutilation (FGM), neglect, and school dropouts are the many cases that mostly occur.

"Early marriages, neglect, FGM, and school dropout are the many cases occurring in the interior and we cannot trace them easily," said the Children's Officer.

He said children's rights violators in the border areas of West Pokot relocate to the neighbouring country of Uganda once they realise that the government wants to pursue them adding that many cases go unreported.

Nyatige appealed to the community to collaborate with the trained CPVs as they perform their duties to protect children against abuse.

"I am calling upon the community members to support the volunteers to help in ending children's rights violations in the region," he appealed.

He revealed that children offices have been opened at sub-counties of Alale and Kacheliba respectively to cut short the long distances travelled when locals are seeking services at the county headquarters in Kapenguria.

"We have other new officers who have been deployed to North Pokot and Kacheliba Sub-Counties. Instead of the locals travelling to Kapenguria, they can get assistance at the Deputy County Commissioners' offices in Alale and Kacheliba respectively," Nyatige said.

He further urged the chiefs and their assistants to actively participate in the child protection campaign and also support the CPVs to unearth any child abuse cases in their areas.

The children's officer lauded World Vision among other partners, for sponsoring the training, noting that they have been at the forefront in supporting the marginalised communities.

Agnes Cheptoo, a beneficiary of the training thanked the government officers for the efforts they have put in to protect children.

REPUBLIC OF KENYA

Kenya Power

## INVITATION TO TENDER

A. Kenya Power invites tenders from interested bidders for provision of the following:-

| TENDER NO. | ITEM DESCRIPTION | TENDER COMMENCEMENT DATE | PRE-BID MEETING DATE | TENDER CLOSING DATE |
|---|---|---|---|---|
| KPI/9A.2/OT/002/HR/23-24 | Provision of Medical Service Provider - Care Management Firm | Wednesday 26.07.2023 | Thursday 03.08.2023 at 10.00 a.m. **(Stima Plaza Auditorium)** | Thursday 10.08.2023 at 10.00 a.m. |

Tender documents detailing the requirements of the above tender may be obtained from the Kenya Power website (**www.kplc.co.ke**) from the **date shown above.**

## CANCELLATION OF TENDER

B. Kenya Power wishes to inform firms participating in the tender below, advertised on **18th July 2023**, that the tender has been **CANCELLED.**

| TENDER NO. | ITEM DESCRIPTION | STATUS |
|---|---|---|
| KP1/6A.1/PT/1/23/B13 | Design, Supply, Installation and Commissioning of Solar Photovoltaic Generation Plants with Associated Power Distribution Network (Mini-Grids) in Mandera, Wajir, Garissa, Tana River, Lamu, Narok, Kilifi and Kwale Counties in Kenya with 7 years O&M Services | CANCELLED |

CANCELLED

The addenda can be obtained on the KPLC portal and website.

**Any inconvenience caused is highly regretted.**

**GENERAL MANAGER**
**SUPPLY CHAIN & LOGISTICS**

**www.kplc.co.ke**

DIAL *977# | Access Kenya Power services fast and easy

REPUBLIC OF KENYA

## Konza Technopolis Development Authority

KONZA Technopolis

## MWALIKO WA ZABUNI

Mamlaka ya Maendeleo ya Konza Technopolis (KoTDA), idara tekelezaji chini ya Wizara ya Habari Mawasiliano na Uchumi wa Dijitali inawaalika mawakala wa bima wenye nia na wanaostahiki kwa zabuni zifuatazo:

| Na. | MAELEZO | NAMBARI YA ZABUNI | DHAMANA | MFUMO | KUFUNGA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Utoaji wa Bima ya Jumla na Bima ya Magari kwa Konza Technopolis | KoTDA/RFP/003/2023-2024 | 100,000 | Wazi | Jumatano, Tarehe 9 Agosti 2023 saa 8.00 mchana |

Wazabuni wanaostahiki wanaweza kupata seti ya hati za zabuni kutoka kwa tovuti ya KoTDA **www.konza.go.ke** kuanzia Jumanne tarehe 25 Julai 2023 hadi Jumatano tarehe 9 Agosti 2023. Wazabuni wanaopakua hati ya zabuni kutoka kwa tovuti watahitajika kutuma barua pepe na maelezo yao ya kina ya mawasiliano kwa **procurement@konza.go.ke** kwa minajili ya kurekodiwa, ufafanuzi zaidi, nyongeza na uidhinishaji wa kiusalama ili kuruhusiwa kuzuru eneo.

Maswali/ufafanuzi wote kuhusu mradi au toleo la kuwasilisha ikiwa ni pamoja na maombi ya kuzuru eneo, yanapaswa kutumwa kwa barua pepe kwa **procurement@konza.go.ke** na kunakiliwa kwa **ceo@konza.go.ke** kufikia Jumanne tarehe 1 Agosti, 2023 saa 1700 saa za Kenya.
Hakuna anwani nyingine za barua pepe zitatumika kwa zabuni hii na KoTDA haitawajibika ikiwa wazabuni watachagua kutuma taarifa zao na/au maswali kwa anwani zingine za barua pepe.

Wazabuni watawasilisha Nakala Moja Halisi na Moja Laini katika Flash drive ya hati zote za zabuni katika bahasha zilizofungwa, zilizoandikwa Nambari ya Zabuni ikiwa imewekewa vizuri kwenye kona ya upande wa kulia na bila kuonyesha jina ya mzabuni na kutumwa kwa:

**Afisa Mkuu Mtendaji**
**Mamlaka ya Maendeleo ya Konza Technopolis**
**S.L.P 1 - 90150,**
**KONZA TECHNOPOLIS, KENYA.**
**Barua pepe; procurement@konza.go.ke na ceo@konza.go.ke**
**Simu; +254-20-4343013/4**

na kuwekwa kwenye Sanduku la Zabuni la KoTDA kwenye Orofa ya 7 ya Konza Complex, Konza Technopolis, iliyo kando ya Barabara ya Nairobi-Mombasa karibu na Mji Mdogo wa Malili ili kufikia anwani iliyo hapo juu kabla ya **Jumatano, 9 Agosti 2023 saa 1400 saa za Kenya.**

Zabuni zilizowasilishwa zitafunguliwa hadharani katika ukumbi huo muda mfupi baadaye mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakaomua kuhudhuria.
Bei zilizotajwa lazima zibaki halali kwa siku Mia Moja na Themanini (180) kuanzia tarehe ya ufunguzi wa Zabuni.

***Ombi la yeyote atakayepatikana akidanganya litafutiliwa mbali***

REPUBLIC OF KENYA

## KENYA UNIVERSITIES AND COLLEGES CENTRAL PLACEMENT SERVICE

ALIGNING CAREERS

### PLACEMENT OF TRAINEES TO KENYA MEDICAL TRAINING COLLEGE PRE-SERVICE COURSES FOR THE SEPTEMBER 2023 INTAKE

The Kenya Universities and Colleges Central Placement Service (KUCCPS) invites interested and qualified individuals to apply for **Kenya Medical Training College (KMTC)** programmes for the **September 2023 intake**.

Holders of KCSE certificate from **2013** to **2022** are eligible to apply.

A list of the available courses, entry requirements, campuses and application instructions are available on the KUCCPS website:**www.kuccps.ac.ke.**
**Katibu wa Idara ya Huduma za Kurekebisha Tabia Salome Muhia atoa mchango kwa mahabusu katika Kodiaga Maximum Prisons, kaunti ya Kisumu. Picha na Chris Mahandara**

"Ninawasihi washirika wengine wote wa maendeleo kujitokeza kuunga mkono mpango wa kupunguza msongamano wa magereza ili kuhakikisha wafungwa wanaishi maisha ya heshima kwa mujibu wa kifungu cha 28 na 43 cha katiba kinachohitaji kila mtu aishi kwa heshima," alisema katika mkutano na waandishi wa habari katika Gereza Kuu la Kodiaga.

Katibu aliongeza kuwa serikali pia itatumia vituo 135 vya probesheni na vituo vya utunzaji vinavyopatikana nchini kote ili kushinikiza mahakama kuwaweka wahalifu wamakosa madogo chini ya huduma ya jamii.

Tatizo la msongamano wa wafungwa huku baadhi ya magereza yakihifadhi maradufu ya uwezo unaotarajiwa limeonekana kuwa chanzo cha hali mbaya ya magereza nchini. Changamoto hiyo imesababisha mzozo wa usimamizi na kuifanya kuwa vigumu kuwakimu wafungwa na mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, huduma za matibabu na huduma za vyoo.

Wakati huo huo, Muhia alifichua kuwa ukarabati wa mfumo wa maji taka katika Gereza Kuu la Kodiaga unaendelea ukiwa katika asilimia 25 na unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba 2023 ili kukabiliana na tatizo la uchafuzi wa mazingira katika eneo hilo.

"Mbali na Kisumu, pia tumeanza ujenzi wa mifumo ya kisasa ya maji taka katika magereza ya Lodwar na Naivasha na tunalenga kusambaza miradi kama hiyo katika vituo vingine vyote nchini kulingana na dhamira yetu ya kukabiliana na tishio la mabadiliko ya hali ya hewa," alisema katibu. Ili kuchangia zaidi katika kukabiliana na athari mbaya za mabadiliko ya hali ya hewa na kuongeza misitu, Idara ya Urekebishaji inanuia kutumia 20% ya ardhi yake kupanda miti bilioni moja kulingana na agizo la Rais William Ruto la kupanda miche ya miti bilioni 15 kufikia 2032."

# Wakulima 252 Kibwezi kutumia sola kuzalisha vyakula

NA PATRICK NYAKUNDI NA RONALD RONO (KNA)

Takriban familia 252 katika Wadi ya Masongaleni katika kaunti ndogo ya Kibwezi Mashariki zitanufaika na Teknolojia ya Kilimo ya Agrivoltaic ambayo inatumika nchini Israel ili kuimarisha utoshelevu wa chakula katika eneo hilo.

Teknolojia ya kilimo ya Agrivoltaic inahusisha kupanda mazao chini ya paneli za sola, na wakati huo huo, kutumia nishati kutoka jua kwa pampu za sola kunyunyuzia mazao.

"Mradi huu utawabadilisha wakulima kutoka kutumia pampu za dizeli kwa kutumia nishati ya jua kuvuta maji kwenye mashamba yao kwa ajili ya unyunyuzaji ili kulima chakula cha familia zao, ustawi na kujipatia kipato kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi," alisema Mkurugenzi wa Taasisi ya Pamoja ya Chakula, Maji, Nishati na Usalama Bi Tania Pons Allon wakati wa hafla ya uzinduzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo katika Shule ya Msingi ya St Patrick Ngomano.

Mradi huo ambao ni wa kwanza kutekelezwa nje ya Israel ulizinduliwa rasmi na Gavana Mutula Kilonzo Mdogo. Unafadhiliwa na Hazina ya Kitaifa ya Kiyahudi-Amerika, Chuo Kikuu cha Arizona, na Taasisi ya Pamoja ya Chakula, Maji, Nishati na Usalama, Arava Valley ya Israel na serikali ya kaunti ya Makueni.

Ujenzi katika eneo hilo utakaokamilika miezi minne ijayo utaboresha kilimo, kutoa nishati na maji kwa shule na jamii inayozunguka na kuongeza ufanisi wa matumizi ya ardhi.

Allon alisema kipindi cha kwanza cha miaka mitatu cha ukuaji kitaanza mara baada ya kukamilika kwa eneo ambapo wakulima watasaidiwa kifedha na usimamizi wa kila siku wa shughuli za kilimo.

MOMBASA WATER
Maji safi maisha bora

**MOMBASA WATER SUPPLY & SANITATION COMPANY LIMITED**

MIKINDANI ST. OFF NKRUMAH RD
P.O BOX 1100-80100
MOMBASA.
Email: info@mombasawater co.ke
www.mombasawater .co.ke

Telephone: +254 041 2222700
Fax No: +254 041 2222728
Mobile: 0726313006
0735655650

## TENDER NOTICE

Mombasa Water Supply & Sanitation Co. Ltd invites eligible firms to apply for the following tender:

| TENDER NO | TENDER DESCRIPTION | TARGET GROUP | TENDER SECURITY | CLOSING DATE |
|---|---|---|---|---|
| MWSS/002/2023-2024 | Provision of Major & Minor Repair Services Motor Vehicles/Cycles | Automotive Garages/Motor Vehicles Dealers | KES 300,000.00 | Thursday, 10th August, 2023 at 11.00am |
| MWSS/003/2023-2024 | Registration of Suppliers | Open | N/A | Friday, 11th August 2023 at 11.00am |

Complete Tender documents ***for Garage services*** can be obtained and downloaded **free of charge** from **www.mombasawater.co.ke**. Bidders who download the tender documents are required to notify Mombasa Water **(procurement@mombasawater.co.ke)** with full contact details for the purpose of receiving any further tender clarifications and/or addendum if need be. These clarifications and addendum will also be posted on our website. Registration of suppliers will be online through; **http://eproc.mombasawater.co.ke/login**

Duly completed tender documents in plain sealed envelopes clearly marked with **tender name** and **number** should be addressed to;

**The Managing Director,
Mombasa Water Supply & Sanitation Co. Ltd,
P.O Box 1100-80100,
Mombasa**

Or deposited in the Tender Box located Outside the Managing Director's office, on or before the specified date above. Tenders will be open immediately thereafter at the company's Boardroom in the presence of tenderers and / or their representatives who may choose to attend.

**MANAGING DIRECTOR**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

KSG
KENYA SCHOOL OF GOVERNMENT

# KENYA SCHOOL OF GOVERNMENT

**Empowering the Public Service**

## EMPLOYMENT OPPORTUNITY

The Kenya School of Government is responsible for developing capacity of public servants within the country and the region through training programs that enhance competencies and skills for higher performance and productivity; expert consultancy services for institutional and business process remodelling for greater efficiency and responsiveness in delivery of services; research to strengthen the scientific basis for policy making and implementation; and articulation of Government programs for enhanced public uptake. These activities and programs aim to transform the Public Service into an innovative, efficient, effective and highly professional agency that is capable of driving implementation of national development agenda. The School comprises five Campuses at Lower Kabete, Baringo, Embu, Matuga and Mombasa as well as four specialized institutes.

The School now seeks a suitably qualified individual to fill the position described below.

| POSITION | REFRENCE NUMBER | NUMBER OF POSITIONS |
|---|---|---|
| DIRECTOR | Ref. KSG/D/02/2023 | 1 |

Detailed information about the post, including duties and responsibilities, requirements for appointment, and application procedure is available at KSG website **www.ksg.ac.ke**. Interested candidates are advised to fill in the prescribed application form and submit by hand delivery, email in PDF or post to the undersigned on or before **Friday August 11, 2023.**

**Director General
Kenya School of Government
P.O Box 23030-00604
Lower Kabete Road
Lower Kabete
NAIROBI
directorgeneral@ksg.ac.ke**

KSG is an equal opportunity employer committed to workplace diversity and gender equality. Minorities, women and persons with disability are therefore encouraged to apply. Any form of canvassing will lead to disqualification. **Only shortlisted candidates will be contacted.**

***Please note that staff-hiring process at KSG is conducted free of any charges.***

KENYA VISION 2030

# NTSA yazindua mpango wa kuboresha usalama wa madereva wa Tuktuk

NA HELLEN LUNALO (KNA)



Madereva wa Tuk Tuk wafuatilia mafunzo kwa makini. Picha na Hellen Lunalo/KNA

Mamlaka ya Kitaifa ya Uchukuzi na Usalama (NTSA) imezindua mpango wa mafunzo unaolenga kutoa ushauri nasaha kwa madereva wa Tuk tuk katika Kaunti ya Kiambu.

Mpango huo uliopewa jina la Usalama Barabarani Elimu na Uhamasishaji unalenga kupunguza ajali za barabarani zinazosababishwa na madereva wa Tuk tuk kwa kuwashirikisha katika shughuli zinazolenga kubadilisha tabia.

Shirika hilo lilisema linakusudia kupatia kipaumbele mafunzo hayo kutokana na ukweli kwamba ajali nyingi zilizotokea hivi karibuni katika eneo hilo zilisababishwa na uzembe wa madereva na hivyo kuna haja ya kuwa na mpango wa uhamasishaji na ushauri.

Naye Meneja wa Usalama Barabarani na Mikakati wa NTSA Samuel Musumba aliwaonya madereva hao dhidi ya tabia ya kutumia kisingizio cha hitilafu za kiufundi za magari baada ya ajali kutokea akisema jukumu ni lao kwa kuwa ndio madereva.

Alikuwa akizungumza wakati wa uzinduzi wa mpango huo katika jengo la kanisa lililoko kwenye Barabara kuu ya Northern Bypass.

"Tumeshirikiana na Polisi wa Kenya na Umoja wa Ulaya katika zoezi hili kwa sababu tulibaini kuwa ajali nyingi husababishwa na kukosa ufahamu kwa dereva au mambo mengine kama vile afya ya akili, matatizo ya kifamilia, uchovu, au ushirikiano mbaya kati ya dereva na abiria wake," Musumba alisema.

Kampeni hiyo ya uhamasishaji inalenga kuboresha usalama barabarani Kiambu, Juja, Ruiru, na Thika kwa kulenga watumiaji wa barabara walio hatarini kama vile madereva wa Tuk Tuk, abiria, wanaotembea kwa miguu, watoto wa shule, miongoni mwa wengine. Masuala ya usalama barabarani yalitiliwa mkazo na wasimamizi wa vyama vya akina na mikopo vya magari ya uchukuzi wa umma wakashauriwa kufuatilia kwa karibu shughuli za wanachama wao ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria na kanuni za barabarani.

---

REPUBLIC OF KENYA

## NORTHERN WATER WORKS DEVELOPMENT AGENCY (NWWDA)

## USAJILI WA WASAMBAZAJI BIDHAA, KAZI NA HUDUMA KWA MWAKA WA KIFEDHA WA 2023-2025

Northern Water Works Development Agency ni mojawapo ya Mamlaka tisa za Ustawishaji wa Kazi za Maji chini ya Wizara ya Maji, Usafi wa Mazingira na Unyunyizaji. Eneo linalosimamiwa na mamlaka ni Kaunti sita ambazo ni Garissa, Wajir, Mandera, Isiolo, Marsabit na Samburu. Mamlaka inasimamia maendeleo, matengenezo na usimamizi wa maji na Usafi wa Mazingira katika maeneo haya.

Ili kuimarisha Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake, tuko katika mchakato wa kutekeleza usajili wa Wasambazaji kwa ajili ya utoaji wa bidhaa, kazi na huduma kwa mwaka wa kifedha wa 2023 - 2025

Waombaji wenye nia na waliohitimu wanaweza kupata taarifa zaidi na kukagua Hati za Usajili/Zabuni kutoka kwa tovuti ya mamlaka: **www.nwwda.go.ke.**

Nyaraka zilizokamilishwa za usajili zilizoambatanishwa katika bahasha zilizofungwa na zilizoandikwa ***"Nambari ya Kitengo na Maelezo ya Kitengo"*** zitawekwa kwenye Sanduku la Zabuni lililoko kwenye **orofa ya chini Chumba A3 - ofisi ya manunuzi, Northern Water Works Development Agency, Maji House, Barabara ya Kismayo, Garissa, ili kupokelewa Agosti 9, 2023 saa 11 asubuhi au kabla ya hapo.**

Anwani ya mahali ya kutuma Maombi
**AFISA MKUU MTENDAJI**
**NORTHERN WATER WORKS DEVELOPMENT AGENCY**
**Maji House, Barabara ya Kismayo**
**SLP 495 – 70100 Garissa, Kenya**
**Simu: +254-46-2103598/3797**
**Barua pepe: info@nwwda.go.ke**

KENYA VISION 2030

---

*In Search of Better Health*

## KENYA MEDICAL RESEARCH INSTITUTE

### REPLACEMENTS

CANCELLED

The Kenya Medical Research Institute (KEMRI) is a State Corporation established in Kenya in 1979 through the Science and Technology (Repealed) Act, Cap 250 of the Laws of Kenya operated under the Science Technology and Innovation Act, 2013 as the national body responsible for carrying out research in human health in Kenya. Currently KEMRI operates under Legal Notice No. 35 of March 2021, the vision is "to be a leading centre of excellence in human health research" and its mission is "to improve human health and quality of life through research, capacity building innovation and service delivery".

KEMRI seeks to recruit dynamic, innovative and experienced persons to fill the following positions:-

Terms of Service: The appointment is on permanent and pensionable terms.

| No | | Job Group | Positions |
|---|---|---|---|
| 1. | Clinical Officer | KMR 8 | 4 |
| 2. | Clinical Psychologist | KMR 6 | 1 |
| 3. | Engineering Technologist | KMR 8 | 2 |
| 4. | Laboratory Analyst | KMR 6 | 2 |
| 5. | Laboratory Technician | KMR 9 | 5 |
| 6. | Laboratory Technologist | KMR 8 | 5 |
| 7. | Senior Clinical Officer | KMR 7 | 1 |
| 8. | Senior Laboratory Analyst | KMR 5 | 3 |
| 9. | Senior Nursing Officer | KMR 5 | 1 |
| 10. | Assistant Principal Clinical Research Scientist | KMR 4 | 3 |
| 11. | Information Scientist | KMR 6 | 2 |
| 12. | Research Scientist | KMR 6 | 2 |
| 13. | Senior Research Scientist | KMR 5 | 1 |
| 14 | Accountant | KMR 6 | 2 |
| 15. | Administrative Officer | KMR 6 | 2 |
| 16. | Assistant Office Administrator | KMR 8 | 2 |
| 17. | Biostatician/Bioinformatics Officer | KMR 6 | 1 |
| 18. | Corporate Communication Assistant | KMR 8 | 1 |
| 19. | Corporate Communications Officer | KMR 6 | 1 |
| 20. | Grants Management Officer | KMR 6 | 1 |
| 21. | Intellectual Property Officer | KMR 6 | 1 |
| 22. | Internal Auditor | KMR 6 | 1 |
| 23. | Legal Officer | KMR 6 | 1 |
| 24. | Planning and Strategy Officer | KMR 6 | 1 |
| 25. | Principal Security Officer | KMR 4 | 1 |
| 26. | Quality Assurance & Risk Officer | KMR 6 | 1 |
| 27. | Research Administrator | KMR 6 | 1 |
| 28. | Senior Assistant Office Administrator | KMR 7 | 1 |
| 29. | Supply Chain Management Assistant | KMR 8 | 2 |
| 30. | Supply Chain Management Officer | KMR 6 | 2 |
| 31. | Driver | KMR 10 | 4 |
| 32. | Cook | KMR 10 | 1 |
| 33. | Office Assistant | KMR 12 | 7 |

All the applications should be done online through KEMRI **Website www.kemri.go.ke/careers - E-Recruitment Portal to be on or before 14th July 2022 latest 5.00 p.m. (East African Time)**

Kindly attach your Curriculum Vitae, cover letter, copies of certified academic and professional certificates, testimonials and other relevant documents.

Please visit the KEMRI web site ***www.kemri.go.ke*** for more details on the advertisement.

Successful candidates will be required to fulfil requirements of Chapter Six of the Constitution.

KEMRI is an equal opportunity employer committed to diversity; persons with disability, women, youth and those from marginalized areas are encouraged to apply. KEMRI does not charge a fee at any stage of its recruitment process including application, interview and processing of offer letter. If asked for a fee, report such request immediately.

Only shortlisted candidates will be contacted.

**DIRECTOR GENERAL**
**KENYA MEDICAL RESEARCH INSTITUTE**

CANCELLED

KENYA VISION 2030

THE BIG 4 EMPOWERING THE NATION

# IRA Board trained on Mwongozo code



Insurance Regulatory Authority (IRA) Board of Directors, led by Board chair Hon. Mwambu Mabongah (3rd right) and CEO Godfrey Kipttum (2nd left) pose with their certificates after successfully completing a training course on the Mwongozo code in Naivasha over the weekend.


KBC
YOUR NATIONAL BROADCASTER

## NOTISI YA TENDA

Kenya Broadcasting Corporation inaalika wale wanaopenda kushiriki kwenye tenda ifuatayo kutuma maombi:

| | |
|---|---|
| **NAMBARI YA TENDA 02/ KBC/2023-24** | **UTOAJI WA HUDUMA ZA USHIRIKIANO KWENYE JUKWAA LA UBORA WA JUU** |

Stakabadhi zote za tenda zinaweza kupakuliwa na wale wanaopenda kushiriki kutoka kwa wavuti wa KBC; **www.kbc.co.ke, tenders.go.ke** au kupokea nakala kamili kutoka Afisi ya Meneja wa Ununuzi katika Broadcasting House Harry Thuku Road. Washiriki watahitajika kujiandikisha kwa kulipa kiasi cha pesa kisichorudishwa cha Sh 1,000 pesa taslimu au hundi ya benki inayolipwa kwa keshia wa Kenya Broadcasting Corporation katika Harry Thuku Road kabla ya tarehe ya mwisho ya kurudisha stakabadhi iliyojazwa (Ksh**.1000/= vijana, akina mama na walemavu hawahitajiki kulipa ada hiyo), washiriki wanaopakua stakabadhi hizo za tenda kutoka kwa mtandao hawahitajiki kulipa bali wanapasa kuwasilisha mara moja maelezo yao kwa ajili ya rekodi na kupokea habari zaidi kuhusu tenda au hata ufafanuzi kwa** afisi ya ununuzi KBC au **procurement@kbc.co.ke.**

Stakabadhi za tenda zilizojazwa zinapasa kuwasilishwa kwenye bahasha iliyofungwa na kuandikwa nambari za tenda na kutumwa kwa :-

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Kenya Broadcasting Corporation,**
**S.L.P 30456-00100, NAIROBI**

**OR**

Iwekwe ndani ya sanduku la tenda lililoko kwenye Lango Kuu katika Broadcasting House mnamo au kabla ya **Agosti 8, 2023** saa **4.00 asubuhi.** Tenda zitafunguliwa papo hapo katika afisi ya Matangazo, KBC mbele ya washiriki au wawakilishi wao ambao wangependa kuhudhuria.

*KBC IS AN ISO 9001:2015 CERTIFIED CORPORATION (CERTIFICATE NO. KE 21/92667)*



REPUBLIC OF KENYA

## PUBLIC SERVICE COMMISSION

**Our Vision**
*"A citizen-centric public service"*

**Our Mission**
*"To reform and transform the public service for efficient and effective service delivery"*

### PROFICIENCY EXAMINATION FOR CLERICAL OFFICERS - AUGUST, 2023.

It is notified for general information that year 2023 Proficiency Examination for Clerical Officers will be held from Monday 28th to Thursday 31st August 2023 at the following examination centres:

| | | |
|---|---|---|
| 1. Nairobi | 2. Nyeri | 3. Mombasa |
| 4. Embu | 5. Garissa | 6. Kisumu |
| 7. Nakuru | 8. Kakamega | 9. Eldoret |

The actual venues will be notified to the candidates after registration.

**ELIGIBILITY FOR REGISTRATION**

To register for the Proficiency Examination for Clerical Officers, an officer must:

(a) Have passed the Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E.) with a mean grade of C – (minus) or its equivalent;
(b) Be designated as a clerical officer in the Public Service; and
(c) Have served as a clerical officer for a minimum period of one (1) year.

**REGISTRATION FEES**

Each candidate will be required to pay registration fees as per the revised rates in the circular **Ref PSC. EXAM/1/VOL.11 dated 3rd May 2018.**

| | |
|---|---|
| **Basic Fee** | **Kshs. 2625** |
| **Fee per paper** | **Kshs. 875 (7 papers)** |

The fee which is non-refundable should be paid in Banker's cheque only payable to P**ublic Service Commission.** Kenya Government cheques, personal cheques, money orders and postal orders will not be accepted.

**REGISTRATION FORMS**

(a) All candidates attempting the examination for the first time are required to complete registration **FORM A** while referred candidates should complete **FORM B.**

(b) The duly completed registration form, accompanied by the correct registration fee should be submitted to the Secretary/Chief Executive, Public Service Commission **P. O. Box 30095-00100 NAIROBI** so as to reach the Commission not later than **10th August, 2023.**

**LATE REGISTRATION**

(a) A **late registration fee of Kshs. 525** will be charged on all candidates who submit their registration forms after **10th August, 2023**. The deadline for late registration is **15th August, 2023.**

This information can also be downloaded from the Public Service Commission website at **www.publicservice.go.ke.**

**DR. SIMON ROTICH, CBS**
**SECRETARY/CHIEF EXECUTIVE**

KENYA VISION 2030



REPUBLIC OF KENYA

**MINISTRY OF MINING, BLUE ECONOMY AND MARITIME AFFAIRS**

***STATE DEPARTMENT FOR BLUE ECONOMY AND FISHERIES***

KEMFSED Enhancing Livelihoods

**KENYA MARINE FISHERIES SOCIOECONOMIC DEVELOPMENT PROJECT (KEMFSED)**
**P O BOX 58187 - 00200 NAIROBI**

**TENDER NO. MMBE&MA/SDBE&F/01/2023-2024**

## INVITATION TO TENDER

The State Department for Blue Economy and Fisheries invites sealed tenders for the supply and delivery of transportation Boats.

Tendering will be conducted under open competitive method National using a standardized tender document. Tendering open to all qualified and interested Tenderers.

**Tenderers will be allowed to tender for Supply and delivery of 4No. Transportation Boats**

Qualified and interested tenderers may obtain further information and inspect the Tender Documents during office hours *0800 to 1600 hour*s at the address given below.

A complete set of tender documents may be purchased or obtained by interested tenders upon payment of a non- re fundable fees of Kshs 1,000 in cash or Banker's Cheque and payable to the address given below. Tender docments may be obtained electronically from the Website **www.mibema.go.ke, www.kemfsed.org,** and **www.tenders.go.ke** Tender documents obtained electronically will be free of charge.

Tender documents may be viewed and downloaded for free from the website **www.mibema.go.ke, www.kemfsed.org; www.tenders.go.ke** Tenderers who download the tender document must forward their particulars immediately to the address below to facilitate any further clarification or addendum.

All Tenders must be accompanied by a tender security of Kenya Shillings ***Three Hundred Thousand Kshs.300,000 from a reputable financial institution***

The Tenderer shall chronologically serialize all pages of the tender documents submitted.

Completed tenders must be delivered to the address below on or before ***17th August, 2023 at 10:00 am***

Electronic Tenders ***will not be*** permitted.

Tenders will be opened immediately after the deadline date and time specified above or any dead line date and time specified later. Tenders will be publicly opened in the presence of the Tenderers' designated representatives who choose to attend.

**Tenders will be open on:**

**NGONG ROAD, MAKTABA KUU BUILDING, MEZZANINE FLOOR, KEMFSED BOARDROOM.**

| | |
|---|---|
| **Physical Address**<br>**The Principal Secretary**<br>**Ministry of Mining, Blue Economy and Maritime Affairs**<br>**State Department for Blue Economy and Fisheries**<br>**Ngong Road, Works Building 3rd Floor**<br>**P O Box 58187 - 00200 NAIROBI**<br>**Email:ps@blueeconomy.go.ke**<br>**Website: https//www.mibema.go.ke** | **Other addresses**<br>**The National Project Coordinator**<br>**Kenya Marine Fisheries and Socio-Economic Development (KEMFSED) Project**<br>**Ministry of Mining, Blue Economy and Maritime Affairs**<br>**State Department for Blue Economy & Fisheries**<br>**Maktaba Kuu Building, Mezannine Floor, Ngong Road,**<br>**www.kemfsed.org, Email: info@kemfsed.org**<br>**Telephone: +254-20-2718870** |

# World Vision, kaunti ya West Pokot kushirikiana kulinda haki za watoto

NA RICHARD MUHAMBE NA MAURICE OSORE (KNA)

Kaunti ya Pokot Magharibi imetoa mafunzo kwa Wafanyakazi wa Kujitolea wa Ulinzi wa Watoto (CPVS) katika jitihada za kuwalinda watoto dhidi ya aina yoyote ya unyanyasaji.

Hatua hii imechukuliwa kutokana na idadi kubwa ya ukiukaji wa haki za watoto unaotokea hasa katika maeneo ya mbali ndani ya kaunti ambapo wenyeji pengine hawataki kuripoti au hawana taarifa kuhusu haki za watoto.

Idara ya Huduma kwa Watoto kwa ushirikiano na World Vision Kenya ilichukua hatua ya kutoa mafunzo na kuwezesha CPV kutoka kila wadi huku asilimia kubwa ikitoka Wadi za Kasei na Sigor.

"Tumewafunza walinzi wa kujitolea watoto (CPVs) 33 ambao wanatoka wadi zote 20 katika Kaunti ya Pokot Magharibi na idadi kubwa kutoka Karsei na Sigor kuhusu jinsi ya kutatua au kushughulikia kesi za unyanyasaji wa watoto," alisema Afisa wa Watoto wa Pokot Magharibi Bw Fredrick Nyatige.



Afisa wa watoto West Pokot, Fredrick Nyatige wakati wa mafunzo kwa maafisa wa kujitolea wa kulinda watoto (CPVs) mnamo Alhamisi Julai 14, 2023. Picha na Richard Muhambe

Nyatige alieleza kuwa ndoa za utotoni, Ukeketaji wa wanawake (FGM), kutelekezwa, na kuacha shule ndizo kesi nyingi zinazotokea.

"Ndoa za utotoni, kutelekezwa, ukeketaji, na kuacha shule ni visa vingi vinavyotokea ndani na hatuwezi kuzifuatilia kwa urahisi," alisema afisa huyo wa watoto. Alisema wanaokiuka haki za watoto katika maeneo ya mpaka wa Pokot Magharibi wanahamia nchi jirani ya Uganda mara tu wanapogundua kuwa serikali inataka kuwafuatilia na kuongeza kuwa kesi nyingi haziripotiwi.

Nyatige alitoa wito kwa jamii kushirikiana na CPVs waliopata mafunzo kwa wanapotekeleza majukumu yao ya kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji.

"Ninatoa wito kwa watu wa jamii kuunga mkono watu wanaojitolea kusaidia kukomesha ukiukaji wa haki za watoto katika kaunti," aliomba.

Alifichua kuwa afisi za watoto zimefunguliwa katika kaunti ndogo za Alale na Kacheliba mtawalia ili kupunguza umbali wanaosafiri wenyeji wakitafuta huduma katika makao makuu ya kaunti hiyo Kapenguria."Tuna maafisa wengine wapya ambao wametumwa katika Kaunti Ndogo za Pokot Kaskazini na Kacheliba. Badala ya wenyeji kusafiri hadi Kapenguria, wanaweza kupata usaidizi katika afisi za Naibu Makamishna wa Kaunti huko Alale na Kacheliba mtawalia," Nyatige alisema.

Aidha, aliwataka machifu na wasaidizi wao kushiriki kikamilifu katika kampeni ya ulinzi wa mtoto na pia kuunga mkono CPV ili kufichua matukio yoyote ya udhalilishaji wa watoto katika maeneo yao.

Afisa huyo wa watoto aliipongeza World Vision miongoni mwa washirika wengine, kwa kufadhili mafunzo hayo, akibainisha kuwa wamekuwa mstari wa mbele kusaidia jamii zilizotengwa.

# MCK yahimiza maafisa kukumbatia vyombo vya habari vipya kuwasiliana

NA ERASTUS GICHOHI (KNA)

Baraza la Vyombo vya Habari nchini (MCK) limetoa wito kwa maafisa wa mawasiliano wa serikali kutumia vyombo vya habari vipya na vinavyoibukia kueleza mipango na ajenda za serikali.

MCK ilisema maendeleo katika teknolojia yamebadilisha sana hali ya vyombo vya habari katika muongo uliopita na kuna haja ya maafisa wa mawasiliano kuoanisha mikakati yao ili kufanikisha zaidi maamuzi ya serikali.

Kulingana na Afisa Mkuu Mtendaji wa MCK Bw David Omwoyo, mawasiliano ya serikali ni sehemu muhimu ya utawala bora na usimamizi wa umma katika utoaji huduma bora kwa wananchi.

Omwoyo, ambaye alikuwa akizungumza mjini Naivasha wakati wa mafunzo ya maafisa wa mawasiliano wa serikali, aliwataka maafisa hao kurekebisha mawasiliano yao kupitia habari zinazoweza kuthibitishwa, takwimu na kuoanisha mikakati yao ndani ya Ajenda ya Serikali ya Kujenga Uchumi kutoka Mashinani. (BETA).

Akizungumza katika hafla hiyo, BwVictor Bwire, Mkurugenzi wa Mafunzo na Maendeleo ya Vyombo vya Habari katika Baraza la Habari alisema kuna haja kubwa kwa maafisa wa mawasiliano wa serikali kuwekeza katika ukusanyaji na usimamizi wa takwimu ili kulandana mabadiliko ya mazingira ya vyombo vya habari. Bwire alisema maafisa wanapaswa kuandika mikakati yao ya mawasiliano kwa kuzingatia raia na kufanikisha masuala ya kitaifa.

Alisema kwa sasa, kuna vituo vya redio vya ndani 220 vilivyosajiliwa na 135 vya televisheni ambapo asilimia 80 kati ya hivyo vinamilikiwa na watu binafsi hivyo ni biashara.

KEBS Kenya Bureau of Standards
Standards for Quality life

Tel: 0206948000 | Toll Free Line 1545 | E-Mail: info@kebs.org | www.kebs.org

## RE-ADVERTISEMENT: VACANCY ANNOUNCEMENT

The Kenya Bureau of standards (KEBS) is a statutory organization of the Government of Kenya established by the Standards Act, Cap 496 of the laws of Kenya in July 1974. The mandate of KEBS is to provide Standardization, Metrology and Conformity Assessment services through Promotion of standardization in commerce and industry, Provision of testing and calibration facilities, Control of the use of standardization marks, undertaking educational work in standardization, Facilitation of the implementation and practical application of standards, Maintenance and dissemination of the International System of Units (SI) of measurements.

KEBS seeks innovative and result oriented individuals to fill the following vacancies,

| S/No | Position | Department | Job Group | No. of Posts |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Director | Human Resource and Administration | 2 | 1 |
| 2. | Chief Manager | Internal Audit | 3 | 1 |
| 3. | Chief Manager | National Quality Institute | 3 | 1 |

**APPLICATION SUBMISSION**

Vacancy details are to be found on KEBS website www.kebs.org under career page. Applications should be addressed to **The Managing Director, Kenya Bureau of Standards, P.O. Box 54974, 00200, Nairobi** and submitted online through KEBS website/portal to be received on or before 17th August 2023. All testimonials MUST be saved starting with applicant's National Identification Number and submitted with the application

**IMPORTANT NOTICE**

i. Upon successful upload and submission of application, the applicant will receive a system generated email notification that the job application details have been successfully submitted.
ii. KEBS DOES NOT charge any fee in the recruitment process.
iii. Persons with disability and female candidates are encouraged to apply.
iv. Academic Qualifications of external origin MUST be accompanied with a recognition and equation certificate from the relevant body in Kenya.
v. Only shortlisted candidates will be contacted. Canvassing will lead to automatic disqualification.
vi. Candidates must comply with requirements of Chapter 6 of The Constitution
vii. **Candidates who had applied for these positions are advised to Re-Apply.**

**MANAGING DIRECTOR**

#WajibikaNaKEBS

Verify the authenticity of KEBS quality marks by use of the KEBS Official Mobile App or sending a text to 20023: SM#Permit Number/ ISM#UCR Number/ DM#Permit Number

**KEBS implements an Anti-bribery Management Policy accessible through KEBS Website www.kebs.org**

www.kebs.org
KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

## OFFICE OF THE DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTIONS

*"Mashtaka yenye Haki na Usawa"*

## INVITATION TO TENDER

The Office of the Director of Public Prosecutions (ODPP) invites sealed tenders from eligible tenderers for the following tenders: -

| S/ No. | Tender No. | Tender Description | Tender Group | Closing |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ODPP/OT/002/2023-2024. | Provision of Cleaning, Sanitary and Fumigation Services for The Office of the Director of Public Prosecutions (NSSF) 19th Floor. | AGPO (YOUTH) | Monday 7th August, 2023 10:00am. |
| 2. | ODPP/OT/001/2023-2024. | Provision of Group Personal Accident (GPA) cover for ODPP. | OPEN | Monday 7th August, 2023 10:00am. |

Interested and eligible bidders may obtain the tender documents and further details on the tender by downloading **free of charge** from the ODPP Website: **www.odpp.go.ke** or public procurement information portal **www.tenders.go.ke.**

Tenderers who have downloaded the tender document must forward their particulars immediately to **procurement@odpp.go.ke/odppprocurement@gmail.com** for the purposes of further communication and issuing addendum if any. Completed tender documents in plain sealed envelopes clearly marked with the tender number should be addressed to:

**OFFICE OF THE DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTIONS**
**P.O. BOX 30701-00100**
**NAIROBI.**

And be deposited in the Tender Box at the **Office of the Director of Public Prosecutions House, along Ragati Road, at the reception during normal working hours from 8.00 am – 12.30 pm and 2.30 pm – 4.50 p.m.** so as to be received on or before **Monday 7th August, 2023 10:00am** Tenders will be opened immediately thereafter in the presence of the tenderers or their representatives who choose to attend at the Office of the Director of Public Prosecutions Boardroom situated at the ODPP House ground floor on **Monday 7th August, 2023 10:00am**

**ASSISTANT DIRECTOR SUPPLY CHAIN MANAGEMENTS SERVICES**
**FOR; DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTION**

KENYA VISION 2030

Find us on: @ODPP_KE www.odpp.go.ke Office of the Director of Public Prosecutions

JULAI 25, 2023

# MyGov.

NAIROBI-KENYA I TOLEO No. 4/2023-2024

A PUBLICATION OF
**Government Advertising Agency**
Telposta Towers, Kenyatta Ave/ Koinange Street
P.O Box 30025-00100,
Nairobi Kenya
Telephone: (+254) 4920000 / 1
E-Mail: info@information.go.ke

# Wakulima wanufaika na mradi wa mifumo ya masoko ya mimea

**NA WANGARI NDIRANGU (KNA)**

Zaidi ya wakulima 300,000 katika kaunti 12 wamepata masoko katika mifumo ya thamani ya kilimo inayojumuisha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na kilimo cha bustani kutoka kwa Mradi wa mifumo ya Soko la Mazao na Maziwa Kenya (KCDMS) ambao ni sehemu ya Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Amerika (USAID).

Mradi wa Mifumo ya Soko la Mazao na Maziwa Kenya (KCDMS) umekuwa ukiendelea nchini kwa miaka mitano iliyopita na pia umeweza kufikia zaidi ya watoto 150,000 walio chini ya miaka miwili na walezi kwa usaidizi wa lishe.

Mradi huo unaomilikiwa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Amerika (USAID) umekuwa ukitekeleza mipango mbalimbali kuongeza uzalishaji na kupunguza umaskini na utapiamlo na pia kuboresha mifumo ya soko la kilimo nchini.

Akizungumza wakati wa hafla ya kiamsha kinywa na wanahabari jijini Nairobi, Dkt Robert Mwadime, Mkuu wa mradi huo alisema, KCDMS ambayo ilianzishwa 2017 na kukamilika Oktoba mwaka jana, haijasaidia tu kupunguza umaskini kwa wakulima wadogo bali pia imeshughulikia uhaba wa chakula nchini.




Judith Odongo pamoja na Robert Mwadime, Chief of Party (CoP) wakizungumzia mradi huo.





Avokado na mbaazi, ni miongoni mwa mazao KSMS imekuwa ikishughulikia na wakulima kuboresha uzalishaji.

"Kwa miaka mitano iliyopita tumekuwa tukishughulika na mifumo tofauti ya thamani hasa ya parachichi, maembe, maziwa, ndizi, karakara na pia shughuli zingine zote za uzalishaji ambazo zinafaidi wakulima katika eneo hili, hasa katika kaunti tisa kutoka eneo la Magharibi na tatu kutoka Mashariki mwa Kenya," alisema.

Dk Mwadime alibainisha kuwa kuhusiana na suala la uzalishaji, wakulima kwa kawaida huwa na chaguo chache sana za kujipatia kipato kwa wanachozalisha na jambo zuri zaidi ni kuwasaidia sio tu katika uzalishaji bali pia kuzalisha kwa ajili ya soko ambayo ni moja ya changamoto kubwa kwao.

"Tunaweza kuwasaidia wakulima kuzalisha zaidi lakini ukosefu wa soko ni changamoto na hivyo ili waweze kuwekeza katika uzalishaji, wamekuwa na uhakika wa soko linalolipa na ambalo ni thabiti," alisema.

Dk Mwadime alisema KCDMS imeweza kutambua masoko na kutoa mfano wa matunda ya parachichi ambayo asilimia 90 yanazalishwa eneo la Kati lakini kupitia mpango huo, zao hilo kwa sasa limeanzishwa eneo la Magharibi.

Dkt Mwadime, alibainisha kuwa ili kuongeza uzalishaji, mradi huo umehakikisha kuwa wakulima wana mbegu bora na kuongeza kuwa serikali za kaunti zinasaidia wakulima kupata mbegu bora pamoja na kushirikiana na sekta ya kibinafsi kama vile shirika la kimataifa la RTI lililounda eneo la miche ili kuhakikisha uzalishaji wa miche zaidi ya 100,000 kwa urahisi.

## KWA UFUPI

### KVDA yasambaza miche 50,000 ya miembe Tot

Mamlaka ya Ustawishaji wa Bonde la Kerio (KVDA), kwa ushirikiano na Serikali ya Kaunti ya Elgeyo Marakwet imeanzisha mradi wa kuimarisha ustawi wa kiuchumi na kuongeza misitu katika eneo hilo kwa kusambaza miche 50,000 ya miembe huko Tot, wadi ya Endo katika Kaunti Ndogo ya Marakwet Mashariki.

Mpango huu wa KVDA ni sehemu ya juhudi kubwa zaidi za kubadilisha Bonde la Kerio kutoka eneo lililokuwa likijulikana kama "Bonde la Kifo" hadi eneo la ufanisi.

Wakati wa zoezi la ugawaji, Katibu wa Idara ya Maeneo Kame, Nusu Kame na Maendeleo ya Kanda Dk Salim Dokota alisema mpango huu unalandana na agizo la rais la kuimarisha misitu nchini kote.

Aidha Dokota alisema wizara imejitolea kupanda miti milioni 60 kupitia mamlaka za maendeleo za kanda katika kipindi cha miaka kumi ijayo.

Alibainisha kuwa wizara inanuia kuzidisha lengo lake la kila mwaka la miti milioni moja katika eneo la Kerio Valley, kwa kupanda miti milioni mbili kila mwaka.

"Zoezi hili ni endelevu na halitaisha baada ya usambazaji mmoja," Dokota alisema na kusisitiza dhamira ya muda mrefu ya kuleta mabadiliko katika bonde hilo.

Alisisitiza zaidi uwezo wa kuleta mabadiliko wa Bonde la Kerio, ambalo kihistoria limejulikana kama "Bonde la Kifo", akisema kuwa kwa mpango huu, eneo hilo litageuka "Bonde la Ufanisi."

Alibainisha kuwa kiini cha kuanzisha kiwanda cha maembe kaunti hilo kinatokana na uwezo wake wa kuwa kichocheo cha uchumi.

"Kwa kuwapatia wakazi wa eneo hilo chanzo endelevu cha mapato kupitia kilimo cha matunda, mpango huo unalenga kuzuia kushirikishwa katika shughuli zisizo halali kama vile migogoro ya silaha. Zaidi ya hayo, mradi huu umewekwa kuchangia pakubwa katika kushughulikia masuala ya mabadiliko ya hali ya hewa katika kanda," Dakota alisema.

Gavana wa Elgeyo Marakwet Wisley Rotich alihakikisha juhudi za utawala wake kukuza kilimo cha mazao ya biashara na maendeleo katika kaunti nzima. Mkurugenzi Mkuu wa KVDA Sammy Naporos alisema kwamba kwamba miche 750,000 ya miembe ilisambazwa kaunti za Samburu, Elgeyo Marakwet, Baringo na Laikipia katika mwaka wa kifedha uliopita.

*Na Rennish Okong'o (KNA)*

### Serikali yatafuta ushirikiano ili kukuza uchumi baharini

Serikali inaendeleza ushirikiano wa kimkakati na mataifa mengine yaliyoendelea katika bahari ili kusaidia kukuza Sekta ya Uchumi wa Baharini nchini ambayo kwa sasa haitumiki kikamilifu.

Akizungumza mjini London, Uingereza, Waziri la Madini, Uchumi wa Baharini na Masuala ya Bahari Bw Salim Mvurya alisema uchumi wa baharini wa Kenya uko chini ya unavyofaa kutumika, na hivyo kuna haja ya kushirikiana na makampuni ya kimataifa ya kuzalisha umeme wa baharini ili kukuza sekta hii ambayo ina uwezo mkubwa wa kuongeza Pato la Taifa(GDP).

Wakati wa mikutano na wawakilishi wa serikali ya Korea Kusini na serikali ya Bahamas, Mvurya na maafisa wa Korea na Bahamas walijadili na kukubaliana juu ya kimkakati ya nchi mbili ikilenga zaidi ushirikiano ulioimarishwa katika sekta wa bahari kati ya nchi zao.

Katika mkutano wake na Balozi wa Bahamas Bw Paul Rolle ambaye pia ni Mwakilishi wa Kudumu wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Baharini (IMO), Balozi huyo alikubali kutoa mafunzo ya safari za baharini kwa makadeti wa Kenya na kutoa fursa za ajira kwa mabaharia wa Kenya katika meli zake za mizigo na meli.

Kwa upande wake, Korea itatia saini makubaliano na Kenya ambayo miongoni mwa mengine yatafungua njia ya kutambua vyeti vya umahiri wa mabaharia kutoka mataifa yote mawili, jambo ambalo litarahisisha uajiri wa mabaharia wa Kenya wanaohitimu kutoka Chuo cha Bandari na kupata fursa katika kampuni za meli za Korea. Makubaliano hayo pia yatawahakikishia makadeti muda wa mafunzo wa baharini katika meli za Korea.

Waziri huyo pia aliwataka wawekezaji wa Korea kujitosa katika sekta ya meli na uvuvi nchini Kenya ambayo alisema kwamba imesalia bila kutumika kikamilifu.

Mvurya aliandamana na Katibu wa Masuala ya Meli na Usafiri wa Baharini Bw Shadrack Mwadime, Mwenyekiti wa Mamlaka ya Usafiri wa Majini nchini Kenya Hamisi Mwaguya na Kaimu Mkurugenzi Mkuu John Omingo.

*Na Julius Ndegwa (PCO)*

# Serikali yazindua mikakati ya kuwezesha wakazi wa makazi ya mabanda kaunti 33

**NA MWANDISHI WA MYGOV**

Serikali inaendelea na mikakati ya kuwawezesha wakazi wanaoishi katika makazi yasiyo rasmi kuishi maisha endelevu na yenye heshima kupitia utoaji wa miundombinu ya usafi wa mazingira na majitaka.

Kulingana na Katibu wa Idara ya Serikali ya Nyumba na Maendeleo ya Miji Bw. Charles Hinga, watafiti wamegundua kwamba kadiri miji inavyokua na idadi ya watu kuongezeka, ndivyo hatari inavyoongezeka pamoja na kuchipuka kwa makazi yasiyo rasmi.

Hinga, katika taarifa kwa MyGov alisema, inakadiriwa kuwa zaidi ya theluthi mbili ya watu duniani wanatarajiwa kuishi katika mazingira ya mijini ifikapo mwaka 2050 huku sehemu kubwa ya ukuaji huu wa miji ikitarajiwa katika miji inayoendelea.

Katibu alibainisha kuwa kupitia Mradi wa Pili wa Uboreshaji wa Makazi yasiyo Rasmi ya Kenya (KISIP2 ambao ni mradi muhimu wa Serikali ya Kenya (GOK) unaotekelezwa kwa ufadhili kutoka kwa Serikali, Benki ya Dunia na Agence Française de Development (AFD), wakazi wa makazi yasiyo rasmi watapewa fursa ya kuishi maisha ya heshima kupitia utoaji wa miundombinu ya msingi ya usafi wa mazingira na barabara za kuyafikia.

Hinga alisema KISP2 imeangaziwa katika ajenda ya Serikali ya kuwezesha wakazi wa makazi yasiyo rasmi ndani ya kaunti zilizochaguliwa kunufaika kupata huduma za kimsingi na usalama wa umiliki wa ardhi na pia kuimarisha uwezo wa kitaasisi kwa uboreshaji wa makazi duni nchini Kenya.

"KISIP2 ambayo kwa sasa inasaidia takriban makazi 200 yasiyo rasmi katika kaunti 33 inalenga kuboresha makazi haya ili kuona maelfu ya wakazi wakinufaika kutokana na uboreshaji wa mtandao wa barabara, maji na usafi wa mazingira endelevu, mitaro ya kuondoa maji ya mvua na udhibiti wa taka, usalama na taa za barabarani na kuimarisha usalama wa umiliki kwa kupanga, kupima na hatimaye kupata hatimiliki,''ilisema katibu.

Mradi huo, Hinga alibainisha, utachangia pakubwa katika kutimiza Lengo la 11 la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs) la miji na jamii endelevu kwa lengo la kuifanya miji kuwa jumuishi, salama, thabiti na endelevu.

Alisema mradi wa KISIP2 pia unatarajiwa kuchangia pakubwa katika kufikia malengo ya Ruwaza ya 2030 ya maendeleo na ajenda ya serikali ya makazi ya bei nafuu.

REPUBLIC OF KENYA
GOVERNMENT ADVERTISING AGENCY
KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD

DESIGN AND EDITING OF MYGOV WEEKLY BY THE KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD
NHIF Building , 4th Floor, P.O. Box 34035-00100
Tel: 0202715390 / 0757029456
Email: info@kenyayearbook.go.ke
www.kenyayearbook.co.ke